REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 28th February, 2023

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

NOTICES OF MOTION

INTRODUCTION OF ANIMAL IDENTIFICATION AND TRACEABILITY SYSTEM FOR ALL LIVESTOCK IN THE COUNTY

Hon. Nicholas Lempaira: Thank you Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT, AWARE THAT agriculture, including crop and animal husbandry is the function of the county Government as stipulated in fourth schedule part two of the constitution of Kenya 2010;

NOTING THAT, Animal Identification and Traceability can be achieved through the use of integrated platforms that will include use of printed and electronic ear tags, data management systems and other approved electronic identification devices;

FURTHER, NOTING THAT the primary purpose of animal identification and traceability systems is to provide information to farmers, service providers and policy-makers, to enable them make informed decisions and to implement suitable plans;

APPRECIATING THAT, these systems benefit a variety of disciplines including: animal and public health and disease control; food safety and quality; market access, trade and economic growth; genetic improvement and productivity and stock theft mitigation;

COGNIZANT THAT, this Strategy will contribute towards conflict resolution, peace and reconciliation and assist the detection and recovery of the stolen animals;

CONCERNED THAT, most of the wards neighbouring Samburu, Baringo and Isiolo have been experiencing cattle rustling, damage of farm crops and loss of lives through illegal migration of the pastoralists from the neighbouring Counties, this House URGES the County Government of Laikipia to consider:

i. Introduction of Animal Identification and Traceability system for all livestock in the County;

ii. Installation of barriers in all migration routes;

iii. Imposition of significant fees and charges to any livestock getting in the County;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

iv. Establishment of enforcement framework for effective procedural performance by the officers assigned.

MOTION

DEVELOPMENT OF SMALL AND MICRO-ENTERPRISES POLICY

Hon. Stephen Ndiritu: Honourable Speaker, I beg to move the following motion;

THAT, AWARE Kenya's economy is largely driven by the informal sector spearheaded by entrepreneurs presenting themselves in form of Small and Micro Enterprises (SMEs);

CONCERNED THAT the informal sector popularly known as the Juakali has different segments and categories spread out in value chains ranging from agriculture, trade, manufacturing, apparels, IT, transport, the creative economy, education among others;

RECOGNIZING THAT, there is need to improve coordination of SMEs through development of an all-inclusive well-structured delivery platform that encompasses multiple solutions and all key stakeholders;

NOTING THAT this sector has a potential to create employment opportunities to over eighty (80) percent of Kenya's working population;

FURTHER NOTING THAT these SMEs have the capacity to leapfrog our nation to a middle-income economy as witnessed in other economies around the world;

RECALLING THAT strong and consistent commitment and political goodwill can deliver the needed growth for the realization of steady and sustainable economic growth;

CONCERNED THAT previous support by the government to this sector has merely been a kneejerk reaction in form of skewed funding and tokenism;

COGNIZANT THAT there exist no unified County policy or legislation in support of the sector and SMEs across the entire value chain; this House URGES the County Government to develop a Policy on Small and Micro-Enterprises (SMEs) detailing recognition, funding, mentoring, expansion, restructuring and marketing of the SMEs products.

Mheshimiwa Spika, nimekuja na huu mswada tuweze kuangazia wale wafanyabiashara wadogowadogo na wanaonekana kama hawana maana katika Kaunti yetu ama nchi yetu. Tulipochaguliwa isipokuwa wale walichaguliwa na chama cha Azimio, tulikuwa tunalenga mama mboga, mtu wa bodaboda, mtu wa mikono na biashara ile kidogo kidogo. Tukasema tunataka kuinua mkulima mdogo tumlete juu ambapo tulikuwa tunasema ni bottom-up.

Kwa hivyo Bwana Spika, ndio maana nimekuja na huu mswada ndio tuungane pamoja. Sisi wote hata kama umekuja na chama gani, jukumu letu kuu ni kuhudumia wananchi wetu kulingana na vile tuliwaahidi tulipokuwa tukifanya kampeni. Najua kila mmoja alikuwa anawahidi wanabiashara vile atashukisha leseni, kuunga mkono biashara zao na hapo tukapenya na kuweza kuja hapa. Haitakuwa jambo la busara kama hatutaweza kuzungumzia wale watu walitupea kura.

Bwana Spika, tuko na hawa watu wanafanya kazi ya Juakali. Hawa watu wanapitia shida mingi. Ukipitia mahali biashara yao inaendelea wanakaa nje. Hawana mahali pa kujificha jua na unaelewa ile kazi yao ni ngumu. Unatimia nyundo, mashine kali ambayo inaweza kuumiza. Huyo mwanabiashara unapata hata serikali haimtabui wala kumsadia ndio aendelee na biashara yake.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Naomba wengine walioko hapa na wanawakilisha wananchi wengine tuungane na tuweze kuja na mpango wa vile tutaweza kuwainua.

Katika idara ya Biashara ambapo niliwahi kuwa mwenyekiti, kwa sasa najua Mheshimiwa Kibue ndiye ameweza kupatiwa hicho cheo, niko na imani atashikilia ile idara. Sisi kama wafanyabiashara na watu ambao wanapata mapato mandogo madogo atahakikisha tumepata ile pesa ya *Enterprise Fund.*

Bwana Spika, unapata badala ya ile pesa kupatiwa mama mboga, inapatiwa mabwenyenye. Watu amabo wanataka mabilioni. Hio pesa inachukuliwa na wachache inaisha. Bunge kama hii ambapo tumechaguliwa na Mungu, najua hata Mheshimiwa Lempaira ni shahidi. Alikuwa anaomba nikifika huko wanikubali na wanipatie kura na ndio maana alifika hapa ili kuweza kutetea hawa *hustler* ambao walimchagua na kuwatendea haki.

Hii ndio maana naomba wakati wowote tutakuwa tunaweka hizo pesa kwa bajeti, Waheshimiwa tuhakikishe wale ambao tunawakilisha mashinani wamefaidika na hizi pesa. Bwana Spika, wale watu ambao wanafanya biashara hapa soko na Juakali si kwamba wote wanatoka hapa, utashangaa ukikuta Mjaluo, Maasai, Samburu na Mkenya yeyote hapo.

Wakati tunazungumzia hawa watu, tunazungumzia wafanyabiashara ambao wametoka kwa kabila mbalimbali katika Nchi ya Kenya. Kila mwananchi yuko na haki ya kuweza kupata hiyo pesa. Bwana Spika, kuna mama mboga ambao wanafanya biashara ndogo ndogo ambao tunafaa tuje na mswada kama huu ambao nimeleta hapa na tuwe na sheria ambayo itaweza kuwasaidia ili waweze kuungwa na serikali ambayo iko mamlakani.

Bwana Spika, ukitoka hapa na uende katika Wadi ya Rumuruti utakuta mama mboga kwa barabara. Kwa hivyo, wakati tunaongea mambo ya wafanyabiashara, sio wale tu ambao wamekusanyika hapa soko. Tuko na mama mboga ambaye anatokea kwa barabara na kuweka kibanda. Huyo mama ameuza kuku ama kitu kidogo na kununua mboga kwa mkulima ili alete hapo aanze kufanya biashara yake.

Huyo mama tunafaa kumshughulikia ili tujue yale ambayo anapitia. Tujue alitoa pesa wapi na ni vipi tutakavyoweza kumsaidia ili aweze kuinuka ndio atoke kwa hiyo barabara na akipata pesa mingi, aende kwa soko kubwa ama atengeneze duka kubwa. Kwa hivyo, naona ni jambo la busara tukiwa tumekuja hapa ili tuweze kuongelea wafanyabiashara wadogo.

Bwana Spika, biashara ni mahali ambapo unategemea ukiuza kitu fulani, mwishowe utapata faida. Ndio maana tunaongea kuhusu wafanyabiashara. Pia ukienda Magharibi mwa Laikipia, wananchi wa huko wanategemea ukulima. Wanalima mahindi, maharagwe, nyanya na aina zingine zozote. Kwa hivyo, ni vizuri tuweze kujua tutasaidia hao watu namna gani ili biashara yao iweze kuendelea hasa kwa wakati huu kuna kiangazi.

Utakuta wale ambao ni wakulima wadogo ambao walikuwa wanategemea maji ya bwawa, bwawa zimekauka. Mboga na nyanya zake zimeisha na hana tumaini. Bwawa ikikauka, inakuwa ni mwisho wake. Tunaomba serikali kwa wakati huu kuna kiangazi, itenge pesa ili wakati wa kiangazi watakuwa na wakati mwafaka wa kuchimba bwawa ili kuwe na maji.

Leo tunalia hakuna maji na serikali imekaa hivyo. Mvua itakuja kunyesha na bwawa ambayo itakuwa na maji kidogo, bado itakuwa na maji kidogo. Ikikaa kwa miezi tatu itakauka na kwa hivyo haitakuwa imesaidia mkulima na mfugaji. Najua kwa wakati huu tuko na shida ya

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mifugo na shida ambayo inatokea Kaskazini mwa Laikipia, inatokea kule kwingine. Sana sana ni kwa sababu ya maji kwa sababu tunasema maji ni uhai na kila mtu yuko na haki ya kupata maji.

Bwana Spika, hata mifugo iko na haki ya kupata maji. Sisi kama Bunge, ni vizuri tuungane na tuweze kusukuma serikali kuweka mikakati ya kuweka pesa za kuweza kusaidia kuchimba mabwawa. Wakati huu kuna kiangazi kwa sababu huu ndio wakati mwafaka wa kusaidia wale ambao wako na mifugo na wakulima.

Kwa hivyo Bwana Spika, naelewa tukiongea mambo ya biashara hakuna Mheshimiwa ambaye yuko hapa na kusema wadi yake haifanyiwi biashara. Mimi nawakilisha watu wa Thingithu ambayo ndio iko na soko kubwa katika Kaunti ya Laikipia nikifuatwa na Nyahururu, Rumuruti, Doldol na Sosian kwa sababu ya soko ya mifugo. Bwana Spika, naomba wale ambao tumechaguliwa tuweze kusaidia wafanyabiashara wadogo.

Bwana Spika, katika *Manifesto* ya Rais wetu, Daktari William Samoei Ruto alisema ya kwamba ni lazima tuwe na viwanda. Hatuwezi kutegemea viwanda vikubwa kama zile ambazo zilikuwa hapa ya Mountex, Rivatex, Mumias na zingine. Si lazima tutegemee viwanda vikubwa. Wananchi ambao wako na mbinu ya kutengeneza ongezeko la dhamani, kama ni nyanya tunalima Rumuruti, Marmanet na Olmoran. Hizo nyanya tukifikia mwezi wa tano tukijaliwa na mvua, nyanya inakuwa mingi na inapotea.

Kama tutakuwa na viwanda vidogo ambazo tutaweka mahali kuna wakulima wa nyanya na viazi tukiwa kama Serikali ya Kaunti, Serikali Kuu ama wafadhili na itasaidia vijana wetu ambao hawana kazi. Hiyo ndio itatusaidia kwa sababu watakuja hapo kutengeneza nyanya na watakuja kutuuzia na pia wale ambao wanapenda *chips* kama Mheshimiwa Leila.

Badala ya kununua katika maduka makubwa ile ambayo hajui inatoka wapi, atanunulia wale wanabiashara wadogo ambao wanatengeneza hizo vitu. Vilevile, najua Waheshimiwa wengi hapa wanapenda *chips* kama Mheshimiwa Gichuki, Mheshimiwa Anthony na Mheshimiwa Kibue. Najua tukiwa na hizo viwanda tutawezesha wananchi ambao wanatengeneza hizo vitu.

Bwana Spika, Katika Kaskazini mwa Laikipia kuna wafugaji na utakuta kuna ng'ombe na mbuzi. Wanafanya ukulima wa mifugo na tunafaa kusaidia watu kama hao. Badala ya ng'ombe zao kununuliwa na madalali ambao wananunua mbuzi elfu mbili, hasa wakati huu wa kiangazi ambapo ng'ombe mzima ananunuliwa elfu tano, tuwapatie morali wa kufanya hiyo biashara.

Tukiwa na kiwanda kama sisi wanalaikipia, kitengenezwe Doldol na kwingineko. Ng'ombe zitanunuliwa hapo na wakati kiangazi inaingia badala ya kutembea mbali na hizo ng'ombe, atakuwa anauza nusu na kutembea na chache ili aokoe pesa yake na jasho yake iweze kumsaidia. Bwana Spika, ukienda Kaskazini mwa Laikipia, kwa sasa utafikiri hakuna ng'ombe na mbuzi kwa sababu wamehama.

Nilipigia Mheshimiwa Leshuel simu kwa sababu yeye ni rafiki yangu ili nijue anaendelea aje. Kwa hiyo simu, nilisikia kondoo wakilia. Mheshimiwa yuko kwenye biashara na nikimpigia kumuuliza yuko wapi, anasema yuko Mlima Kenya ilhali kwake ni hapa. Najua yale ambayo wafugaji wanapitia na tukiweza kuwasaidia, yeye ni mmoja wa wale ambao wako hapo.

Kila wakati huwa nasimama kusema tuwasaidie wafugaji, yeye atakuwa mstari wa mbele kuhakikisha ya kwamba wale ambao wako hiyo sehemu wamesaidika. Huu ndio wakati mwafaka

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ambapo najua ataunga mkono ili tuweze kuwasaidia wakulima wadogo ambao wanafanya biashara ya ufugaji.

Bwana Spika, Elimu ndio msingi wa maisha na bila elimu maisha inakuwa ngumu. Ni vizuri Bunge la Laikipia liweze kusaidia serikali iliyoko na kuisukuma ili iweze kuhakikisha ya kwamba wananchi wetu wamepata elimu bora. Elimu si elimu tu mbali ni elimu bora.

Serikali ya Kaunti iko na jukumu la kuhakikisha ya kwamba tumetengeneza madarasa ya chekechea kwa sababu hapo ndipo mtoto anaanza. Wakati unafanya bajeti hapa, ni vizuri Waheshimiwa katika Bunge hili wapatie kipaumbele madarasa ya watoto wa chekechea kwa sababu huyo mtoto ndio anaanza kukua. Tukimuunga mkono tutakuwa tumeunga mkono familia, nchi na kanisa na nchi itakuwa imeendelea.

Bwana Spika, leo najua kuna sehemu zingine ukienda, utapata watoto wanasomea mahali ambapo huwezi taka kukaa. Pia wewe Bwana Spika huwezi furahia. Unakuta mahali mtoto anasomea, akiwa ndani ni kama yuko nje kwa sababu unamuona na ni mtoto mdogo. Kuna mianya na mvua ikinyesha huyo mtoto ananyeshewa akiwa ndani mpaka saa zingine huenda tukapata laana ya hao watoto.

Naomba Bunge hili iweke pesa ya kutosha katika Idara ya Elimu ili tuwaunge mkono watoto ili waweze kupata elimu bora na tuweze kuwasaidia. Najua kuna sehemu zingine watoto wanasomea chini ya mti na ni wachanga. Hakuna madarasa. Najua tuko na majukumu na tuko na nafasi nzuri ya kuweza kutengeneza Kaunti ya Laikipia ili tusaidie wananchi.

Bwana Spika, tukienda upande wa viwanda, Wadi ambayo nawakilisha iko na mashamba ambayo imetengwa ya kutengeneza viwanda lakini kwa bahati mbaya, matajiri ambao wako na pesa wameweza kunyakua hayo mashamba. Wameweza kubadilisha ikawa sasa inajengwa manyumba ya kukodisha. Bunge la Laikipia linafaa kuangalia vizuri ili wahakikishe ya kwamba mashamba ambayo yanatengewa viwanda yamelindwa.

Nikiwa peke yangu nitapiga makelele ili mashamba yasiende na huenda nisifaulu lakini tukishikana na Mheshimiwa Theuri, John, Moile na Leila kwa sababu napenda kuzingirwa na mashujaa, tutapata hayo mashamba kwa haraka.

Huenda tukapata hayo mashamba haraka haraka. Juzi tu, mwaka uliopita niliweza kurudisha shamba la soko. Hicho hakikuwa kitu rahisi, nilikuwa karibu kufungwa. Karibu nife. Nagusishwa bunduki, ni vile tu mimi ni kama ndume, nilienda mtoni. Nilipambana na wale wahalifu na kuweza kuhakikisha ya kwamba tumepata hilo shamba.

Kwa hivyo nawaomba hawa Wabunge wote tuungane sote pamoja ili tuweze kuenda moja kwa moja tuokoe hayo mashamba. Uwanja wa Nanyuki umeenda, imebaki tu kidogo. Walionyakua wako hapa tu wanatembea, lakini sasa mimi nikienda kupigania najikuta nimepelekwa jela. Nakumbuka wakati ule mwingine nilitolewa na akina Cate baada ya kufungwa. Uzuri ni kwamba sikufikisha siku nane, nilikaa siku mbili nikatolewa.

Mimi natetea haki ya wananchi na najua kwenye kila wadi, hayo mambo yanaendelea. Ukienda Rumuruti unapata mashamba mengine yamenyakuliwa. Ukienda Wadi ya Nanyuki, yamenyakuliwa. Hata huko Doldol, huyu Lempaira wakiwa na Shuel wanaweza kutuambia pengine mengine yameenda. Kwa hivyo, tuungane na kukaa pamoja ili tuweze kuwasaidia wale wanaofaa kusaidika. Kwa hivyo, mimi naona nimeweza kuleta mswada utakaosaidia watu wetu,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mahustler, mama mboga na kila mwananchi aliye na moyo mzuri wa kufanya biashara katika Kaunti yetu ya Laikipia. Tunaomba pia serikali ifanye haraka ili tuweze kuwasaidia hawa wananchi.

Bwana Spika, kuna hili jambo la kuwa na *political goodwill.* Hiyo ni yetu, Gavana akiwa hapo, pamoja na Rais, Seneta na sisi wote. Kukiwa na *political goodwill* tutaweza kuwasaidia hawa *mahustler.* Nami namwomba Rais wetu, kwa sababu tulikuwa tunaongea mambo ya mama mboga, *hustler* na mtu wa bodaboda, hata yeye atakapo kuwa akiwateua *CAS*, awakumbuke akina mama mboga. Tunataka kuona mama ambaye alikuwa anauza mboga angalau amepata hicho kiti. Hata yeye hawezi kujikuna akikalia hicho kiti. Tutakuwa tumemsaidia na kuweza kuona kweli mama mboga amepata hicho kiti.

Siku hizi unapata kuwa wale wanaojiita mama mboga ni akina Kosgei. Eti mimi nikifanya nampa Kosgei. Nimempata Kosgei hapa akifanya kazi yake. Iende kwa yule mama mboga anayechomeka pale ndio tuweze kuwaonyesha wananchi ya kwamba sisi tunawajali *mahustler*, mama mboga na watu wa bodaboda. Hii haina ukabila wala mipaka ya vyama. Ni tukae pamoja na kuungana. Kwa hayo machache, ninaomba hawa Waheshimiwa wote waunge huu mswada mkono na kuupitisha ili tuweze kuwasaidia wananchi. Nataka kumwalika Mheshimiwa Umija ambaye pia ni Kiranja wa Walio Wachache kuuafiki huu mswada. Asante.

Speaker: Thank you, Hon. Stephen. As she rises to support and second the motion, I would like to let you know that you might have noticed in your gadgets that our e-parliament has a hitch. That is why you have been given hardcopies. Kindly use the hardcopies. Welcome, Hon. Umija.

Hon. Catherine Umija: Thank you, Mr. Speaker. I would like to second the motion prepared by Hon. Stephen. I just want to support the development of the policy of the SMEs in Laikipia County, noting that they contribute more than 60% of the GDP in Laikipia County. So it is important that we develop policies that are more friendly to them considering that doing business in Kenya, according to the World Bank 2017, takes around 22% of income per capita for somebody to start a business. Therefore, it is important that we do these policies so that it is easier for these SMEs to start business and thus it will help people to create more employment in Laikipia County. Thank you and I support.

Speaker: Thank you, Hon. Stephen Ndiritu and Hon. Catherine Umija.

(Question proposed)

Speaker: For the motion, the floor is open for contributions.

Hon. John Gichuki: Asante, Bwana Spika. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa wa Thingithu kwa kuleta huu mswada. Nikiangalia vizuri, huu mswada unagusa wale wafanyibiashara wadogo wadogo. Watu wako na ujuzi wa biashara, shida yao kubwa ni pesa. Mimi kama Kiongozi wa Walio Wengi naweza tu kuomba hii serikali yetu iangalie sana na kuwafadhili wafanyibiashara wadogo wadogo.

Bwana Spika, kuna siku moja nilienda kwenye soko ya mbuzi nikapata kijana mmoja ananunua mbuzi na kuwafunga pale kando kisha anaenda kuwauza. Nilimuuliza maswali akaniambia yeye huenda kuchukua pesa, elfu hamsini kutoka kwa mtu na kumwambia kuwa atarudisha pamoja na elfu tano zaidi ifikapo jioni. Kwa hivyo, lazima aende kununua mbuzi na

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ahakikishe amewauza siku hiyo hiyo. Mimi ningeomba serikali iingilie kati iwape hio pesa, walipe polepole na waweze kufanya biashara.

Tukienda upande wa wakulima, tuko na wakulima wadogo wadogo ambao baadhi yao wanalima nyanya kama kwenye eneo langu la Rumuruti. Kuna wanaolima ekari moja ama nusu ekari. Unapata kuwa mtu ameweka elfu hamsini zake pale kwenye shamba na kulima nyanya pamoja na kuzipiga dawa, ila mwishowe anashindwa kwa ajili ya kukosa pesa za kumalizia. Hiyo shamba ingekuwa na uwezo wa kumpa elfu mia mbili baada ya kufanya kazi na elfu hamsini au sabini, lakini kwa sababu ya kukosa pesa ya kumalizia kwa kupiga dawa na kuweka maji, huyo mtu anapoteza pesa yake kidogo aliyokuwa nayo.

Kupitia shirika la ukulima, huyo mkulima kama angepewa pesa kidogo, ama kukiwa na mpangilio wa kupewa pesa anayoweza kulipa polepole ingemwezesha kupata pesa na pengine angekopa mara moja na hangewahi kukopa tena. Ningeomba tu serikali iingilie kati, wengi ni vijana wanaofanya hizo kazi ndogo ndogo; iwape pesa kupitia mashirika yote. Kama ni wa bodaboda wapewe pesa kupitia shirika la bodaboda, kama ni wakulima ipitie shirika la ukulima. Kama ni wafugaji, kuwe na pesa ambayo dalali anaweza kuchukua na kufanyisha kazi kisha alipe polepole. Mimi ningeomba hilo. Pesa ama mikopo ipatikane ili watu wetu waweze kufanya biashara ndogo ndogo.

Lingine ni kuwahamasisha kupitia masomo. Hao wakulima wanastahili kupewa masomo. Huenda ana pesa bali hana masomo. Afundishwe jinsi ya kufanya ukulima, kama anataka kulima nyanya apewe mafunzo ya ukulima wa nyanya. Kama ni vitunguu apewe masomo ya ukulima wa vitunguu. Kama ni mambo ya mbuzi, akalishwe chini aambiwe kwamba anafanya biashara nzuri ila inatakikana afuate mpangilio fulani. Tukifanya hivyo hawa watu hawatapoteza pesa zao. Hakuna siku watawahi kupoteza pesa zao.

Unapata mkulima ametumia kama elfu sabini kulima lakini kwa vile hana ujuzi wa kuua wadudu wanaoharibu nyanya, anapoteza hiyo pesa yote. Ningeomba wapate pesa na wakati huo huo wapate mafunzo. Serikali ikifanya hivyo tutakuwa tumetekeleza ile ajenda yetu ya *bottom-up* yenye tulienda tukitangaza kama watu wa UDA. Asante na tuwe na jioni njema.

Speaker: Thank you, Hon. John Gichuki Maina. I now want to give this opportunity to Hon. Mugambi Gatati.

Hon. Samuel Mugambi: Thank you, Mr. Speaker, for giving me this chance. I am standing on support of the timely motion by Hon. Kagondu on promotion of small and micro enterprises in areas such as recognition, funding, mentoring, expansion, restructuring and marketing of SMEs products. I want to put up a good statement, and this motion is timely since last week we heard from our Governor that the National Government gave our county Kshs.100 million for an industrial park. I also think that when you are talking about an industrial park, it is another channel where our micro and small industries will go and expand their industries there.

This is also another channel whereby our small and micro enterprises will go and expand their businesses. The Governor insisted that as a county, we shall also add another a hundred million so that is a total of Kshs.200 million. I would like to urge this House that when it comes to giving out this money and in the building of the industrial park, we need to identify the special groups , the youths , women and PWDs in this funding. We also need to give them places and forums to do business because Mr. Speaker, SMES contribute 80% of our GDP in this country.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Most of the people earn money out of being in this small business. If you go to the bodaboda sector, it has a very big potential but it is not tapped. I think we as the House need to come clean and come up with more motions on how we can support and develop small sectors like the bodaboda. We have others like salons and barbers that are done by small and micro enterprises and most Kenyans depends on these businesses. This is a very timely motion and I think as I sit down, we need to confirm whether these motions discussed here are given an ear by the Executive. We may have good motions, discuss and pass time but when forwarded to the Executive, nothing is implemented.

I think I would urge the House and the Committee on Implementation should also follow up on that and be more serious. I think the committee should be giving us some quarterly reports on how the motions that we have so far discussed are implemented. Thank you Mr. Speaker, for giving me this chance.

Speaker: Thank you Hon. Mugambi Gatati. I want to urge the Members to continue contributing. The floor is still open.

Hon. Paul Leshuel. Thank your Mr. Speaker. I also stand to support this motion and I want to celebrate the Member for Thingithu for bringing this motion. The motion is a very nice motion but we need to address few issues on this so that it can be possible to implement them. We also need as much as we bringing a motion to this House, we need to look into areas of budgeting. We need to have a budget because if we think about the small groups and small enterprises, how much have we allocated for that? That's the key. We need to look into the budget properly so that we don't pass motions here and realize later we have not allocated money for those areas.

Mr. Speaker, we need also to see the policies because policies also limit other people to benefit. I can give an example, in some groups you realize the policies say you give a six months statement so that you can get the small amount of money. How many groups are active to an extent they are saving money? For your information, they do not have money to save. Those are the limitations; we must look at the policies properly so that they do not limit our people from accessing the funds. We need also to come up with many policies to realize the bottom up.

I know most of the governments implement 30% to 40% of its manifesto. It might be very difficult to implement 50%. I can tell but now with the 30% to 20% that we are targeting the small group in the bottom up model, we need to have proper policies that will make us realize that the small people down there have been checked. If you tell us that *mama mboga* probably gets THE CECM or PS. You know the limitations. It is like what we are saying, we need a person with an experience of ten years.

How do you expect a student from university to have the ten years' experience? He might be jobless for five years, so the experience limits them to get a job. There are a lot of factors that we need to think about as a House so that we don't limit our people from benefitting or limit the government from implementing the manifesto

The motion is nice but we must work beyond this motion so that we can be able to put policies in place, to put our budget in place and to put the government in order so that they can be able to implement. I am the Chair of the Implementation Committee and I am sure I will bring to this House the report that will give us the guidelines. What is the percentage of the motion that is implemented in the executive side? What are the challenges? Is it that we do not have a budget or

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

we are approving things that are impossible to be implemented? I am sure we will come up with the report. Mr. Speaker I want to appreciate the Members. There is what we call value addition. It needs money allocation.

Mr. Speaker, if today you go to a certain farm and buy some onions, you will get the unions for Kshs.20 shillings per kg. As a farmer, if you calculate the cost of the same onion until harvesting, it costs you Kshs.25 shillings per kg. Now we are losing five shillings per every kg. If you come to the market here, you will buy at 80 or 60 shillings. So the difference is taken out by the brokers. You will find that when the onions and tomatoes are ready, you have nowhere to put them until you get the market. So definitely, you will have to sell them on the exact day.

Those are the challenges that we need to address and put in place ways of value addition so that if I don't want to sell my onions today, I will have other ways that will enable me to look for markets probably for next week or next month. I want to support and tell the Hon. Members that without supporting the *mama mbogas* and the small people down there, the economy will not grow.

There are so many youth in our areas especially in Laikipia North who have the ability and the capacity to buy animals in auctions and sell in Nanyuki but the challenge is the capital. The moment you put capital in place and put good policies to access that money, they can do a lot. I want to tell the House that we need to look at this holistically so that we can be able to move without many challenges. Thank you.

Speaker: Thank you, Hon. Leshuel for the robust contribution. The floor is still open for the Members to continue contributing.

(Silence)

I will now call upon the mover of the motion to reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Kwanza nataka kushukuru Wajumbe kwa sababu wameweza kutoa maoni yao na kuweza kuunga huu mswada ambao kwa kweli utaweza kusaidia wananchi kama utaweza kufuatiliwa na kufanyishwa kazi na Serikali ya Kaunti.

Jambo ambalo ningetaka kusema ni ya kwamba Serikali Kuu imeweza kuonyesha nia njema kuweza kusaidia wakulima wadogo, hasa wale ambao wanaofanya bishara ndogo. Kwa mfano, wakati Rais alipokuwa ametembea Nanyuki aliahidi ya kwamba ataweza kutengeneza soko ya Nanyuki Old Market na sasa najua ya kwamba hatua imeanza kupigwa. Waziri alitembea hapa na pia Gavana ametembea kwa hiyo soko na kuweza kuiangalia.

Tungetaka pia Serikali ya Kaunti zile soko zilizoko pande za Rumuruti, Likii, Matanya, Ngobit, Mukogodo zote mbili kwa sababu hata Chumvi kuna soko na Mheshimiwa Leshuel ameweza kusema tusaidie hao wanabiashara wadogo. Nayo Serikali ya Kaunti tuweze kusikia ya kwamba wametengeneza soko ingine huko nje ndio tuweze kusaidia wale wakulima wadogo wadogo.

Bwana Spika, ningetaka kumwarifu Mheshimiwa Shuel kwa sababu ameongea kuhusu kina mama mboga na kwa sababu najua ya kwamba yeye hupenda watu wa *bottom up,* mkokoteni na boda boda. Hata ukimuangalia anakaa kama mtu *wa hustler nation* ingawaje aliiingia akiwa mtu wa *independent*, lakini alipofika hapa ameweza kuangukia upande wa *hustler*. Niweze kumkumbusha na kumueleza ya kwamba wale kina mama mboga ambao wako huko wako na ujuzi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

na pia wamesoma na kupata shahada na ni kazi tu wamekosa. Unapata huko kina mama wamepata *masters* lakini wanauza mboga kwa sababu kazi zilikosa. Wengi wako na ujuzi na masomo na ni vile tu hawajapata nafasi ya kutumikia wananchi.

Kwa hivyo, mimi naweza kuwa shahidi kwa sababu nimekaa kwa soko zaidi ya miaka kumi na ninajua wale watu ambao wako huko. Wengine wamesoma mpaka wakafika mahali pameandikwa *no school ahead* na wako huko. Kwa hivyo, wale watu ambao wamesoma wanajua na kuelewa haya mambo ya kujipanga.

Mimi nilipoona Shuel mara ya kwanza kwa sababu maana sikuwa namjua, nilipita huko chumvi pande ya chini na kupata mtu ambaye amevalia shuka, viatu za ngozi na nikafikiri yeye ni mtu tu wa kuchunga lakini sikujua ya kwamba yeye ni mtu ambaye yuko na ujuzi na pia ni Mheshimiwa, lakini wakati mwingine anafanya ile kazi ambayo imepatikana. Ukimpata pale, utafikiria ya kwamba hajasoma lakini amesoma na yuko na ujuzi na pia amefanya hadi na NGOs. Nataka kusema ya kwamba wale ambao wako huko wako na ujuzi wa kutosha na tukiweza kuwasaidia na kuwainua vizuri inavyostahili.

Vijana wetu pia, vile amesema ni ukweli. Wengi wanaweza kukosa ujuzi lakini tunaweza kujaribu vile tutawasaidia na ndio maana tunatengeneza viwanda na vinginevyo. Kwa hivyo, tutawapeleka pale na waweze kupata huo ujuzi. Mimi ninajua ya kwamba kijana kama wa Shuel amesoma na sasa hivi kile kitu ambacho anahitaji ni ujuzi. Hao vijana tukiwachukua tuwaweke mahali pamoja ambapo watakuwa wakifanya mambo kulingana na masomo yao, katika mwaka mmoja ama miwili watakuwa na ujuzi.

Tuombe serikali hii yetu ya Kaunti kwa sababu tunataka kuunga wale vijana tuwapatie *internship* ili waweze kupata ujuzi na tutaweza kuwasaidia. Ninashukuru hasa Mheshimiwa Shuel kwa kuchangia mswada ambao ameona ya kwamba utaweza kusaidia watu wake na ndio maana alitumwa hapa. Namshukuru Mheshimiwa Gatati pia maana ameweza kuchukua huu mswada na kuuweka vile unavyostahili.

Mimi najua ya kwamba Mheshimiwa Gatati anaelewa mambo ya biashara na kwa hivyo, wakati amesimama hivyo na kuchangia, hata nilikuwa nafikiria kwamba yeye ni mmoja wa wale ambao tunaweza kusaidia awe laini ya mbele kuhakikisha ya kwamba tumetengeneza viwanda. Yeye ni kijana, anajali vijana na pia anaelewa shida ambazo vijana wanapitia. Kila wakati mimi humuona akisaidia vijana. Kwa hivyo, tunataka wajumbe ambao wako na hiyo nguvu na ukakamavu wa kusimama na kutetea watu wao.

Hawa wajumbe wote ambao wako hapa, mimi najua ya kwamba kila mtu yuko na nia njema na wananchi. Hata kama hatujapata nafasi ya kuongea, ninajua kila mmoja hapa katika mioyo yao wameongea kabisa. Mheshimiwa Gichuki ameongea, Mheshimiwa Theuri pia ameongea. Ukiona amenyamaza hivyo, ninajua ya kwamba kile kitu ambacho tunaongea hapa ni kile tu ambacho nataka pale kwake Likii. Mheshimiwa Cate vile vile, Mheshimiwa wa kutoka Githiga huko kote wanalima nyanya na Mheshimiwa Mwaniki hapa anajua mambo ya biashara. Mheshimiwa Moile vile vile anaelewa ya kwamba haya mambo ni kujipanga.

Nimefurahi kwa sababu Mheshimiwa Umija ndiye ameweza kuafiki huu mswada wa *bottom up* na kwa hivyo, inaonyesha ya kwamba sisi wote tuko ndani na ni vile tu tuliingia kwa milengo tofauti. Anajali sana watu wa biashara na ndio maana unaona akisema ya kwamba atawang'oa wale matajiri na awakate shingo ambao hawataki kina mama mboga *na hustler nation*

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wakiinuka. Kwa hayo machache, ninaunga mkono na kuwashukuru kwa vile mmeweza kuleta huu mswada.

Namshukuru rafiki wangu pia, Kiongozi wa Walio Wachache kwa ukakamavu wake na pia kutetea wale walioko chini. Yeye mwenyewe ametoka Thingithu ambapo kuna watu wengi ambao wanataka kusaidiwa. Hii ni nafasi ambayo tutakayotumia mimi na yeye kusaidia wale watu ambo wako katika hii wadi yetu. Sasa hivi, hata tumeweka kando milengo kama Azimio na UDA lakini tuko huko ndani ili kuhakikisha ya kwamba mambo yote yanaendelea. Anaendelea akiwa Azimio na mimi nikiwa upande wa *hustler nation.* Asante.

Speaker: Hon. Stephen Ndiritu, congratulations for a robust reply.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: This House now stands adjourned until tomorrow Wednesday, 1st February, 2023.

The House rose at 3.30 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*